**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA KUNAWA MIKONO DUNIANI

**DODOMA: 15 Oktoba, 2025**

Leo tarehe 15 Oktoba, 2025 Tanzania inaungana na mataifa mengine Duniani katika kuadhimisha **Siku ya Kunawa Mikono Duniani.** Siku hii hutumika kutoa elimu na kuhamasisha jamii kudumisha tabia chanya ya kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni kama njia madhubuti na rahisi katika kudhibiti magonjwa yanayoweza kuenezwa na mikono iliyochafuliwa na vimelea mbalimbali vya magonjwa.

Baadhi ya magonjwa yanayoweza kudhibitiwa kwa kuzingatia unawaji wa mikono kwa maji tiririka na sabuni mara kwa mara ni pamoja na marburg, ebola, UVIKO-19, magonjwa ya macho, kipindupindu na magonjwa mengine ya kuhara.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Kunawa Mikono kwa mwaka huu ni **"kuwa shujaa wa kunawa mikono".** Kaulimbiu hii inalenga kuhimiza mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kuzingatia na kudumisha tabia chanya ya kunawa mikono kwa nyakati zote muhimu ambazo ni kabla ya kutayarisha chakula, kabla ya kula au kumlisha mtoto, baada ya kutoka chooni na baada ya kumsafisha mtoto.

Serikali kupitia Wizara ya Afya inatekeleza shughuli mbalimbali za Afya Mazingira kama vile kuendesha Kampeni ya **Mtu ni Afya** ambayo moja ya malengo yake ni kuhamasisha unawaji wa mikono kwa kutumia maji tiririka na sabuni katika ngazi ya kaya, taasisi na maeneo ya umma yenye mikusanyiko ya watu. Kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ugonjwa wa kipindupindu umedhibitiwa katika mikoa 24 iliyowahi kukumbwa na ugonjwa huo kati ya 26 ya Tanzania bara na mpaka sasa hakuna halmashauri yenye ugonjwa huo.

Aidha, Mfumo wa Wizara wa Utoaji Taarifa za Magonjwa (IDSR) umeonesha idadi ya watu wenye magonjwa ya kuhara wanaokwenda kwenye vituo imepungua kwa asilimia takribani **76%** kwa kipindi cha miaka mitano (5) kutoka wagonjwa **960,956** kwa mwaka 2020 hadi wagonjwa **223,714** kwa mwaka 2025.

Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa Huduma Endelevu za Maji na Usafi wa Mazingira kwa kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji, vyoo na vifaa vya kunawia mikono katika vituo vya kutolea huduma za afya na shule za msingi nchini. Jumla ya vituo **2,957** na shule **2,125** katika mikoa 25 ya Tanzania Bara vimenufaika.

Ikumbukwe kwamba ''**Kinga Ni Bora Kuliko Tiba''** hivyo Wizara inatoa wito kwa wananchi kuendelea kudumisha tabia ya kunawa mikono nyakati zote muhimu ili kujikinga na magonjwa ya kuambukiza.

Imetolewa na:

**Dkt. Grace.Magembe**
**MGANGA MKUU WA SERIKALI**